OFISI YA RAIS TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

SHULE YA SEKONDARI GABADAW

S.L.P 27,

KATESH- HANANG.

…….

KMB.NA GBD/SS/JINSTR/2020/01

JINA LA MWANAFUNZI:……..

S.L.P…….

Ndugu,

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GABADAW MWAKA 2021

1.0. UTANGULIZI

Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2021 Shule ya Sekondari Gabadaw.Shule ya Sekondari Gabadaw iko umbali wa km 14 magharibi mwa mji mkuu wa wilaya ya Hanang (Katesh).Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 hivyo unatakiwa kuripoti shuleni tahere 11/01/2021 bila kukosa saa moja kamili asubuhi.
Na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 endapo hutaripoti kwa muda uliotajwa hapo nafasi yako atapewa mwanafunzi mwingine aliyefaulu.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. SARE YA SHULE (IFANANE KWA RANGI,MISHONO NA UBORA WAKE)

A. SARE ZA WASICHANA

- Sketi mbili za rangi ya kaki na kiwe ni kitambaa cha material' namba moja.
- Sketi ziwe ndefu zisizoonesha maungo,kitambaa kiwe kizito, Sketi ziwe rinda box.
- Blauzi mbili nyeupe(shati ya shule) aina ya tetroni zenye mikono mifupi.
- Sweta rangi ya Zambarau.
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu wala urembo na vyenye kamba(gidamu).
- Stocking/soksi ndefu nyeupe.
- Raba nyeupe kwa ajili ya michezo,Bucta ya blue na Tracksuit kijani yenye mistari nyeupe pembeni.
- Mfuko wa kubebea madaftari na vitabu.
- Wanafunzi wa Kiislamu wavae hijabu ya vitambaa vilivyotajwa hapo juu.

B. **SARE ZA WAVULANA**

Suruali mbili za rangi ya kaki zenye rinda mbili mbele kila upande, zisiwe mnyonyo au "model". Kitambaa kiwe kizito, namba moja.

- Sweta rangi ya Zambarau.
- Mashati mawili meupe ya tetroni ya mikono mifupi
- Raba jozi moja nyeupe kwa ajili ya michezo.
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu wala urembo na vyenye kamba (gidamu).
- Stocking/socksi ndefu za kaki jozi mbili.
- Mfuko wa kubebea madaftari na vitabu.

2.2. VIFAA VYA DARASANI NA CHAKULA.

- Kila mwanafunzi aje na madaftari makubwa Counter Q3 kumi, Kalamu,Mkebe wa hisabati,Rula na Penseli.
- Kamusi (iwe ya Kiingereza tu na Ream 1 kwa matumizi yamitihani yake.

Mahitaji menigne muhimu ambayo mwanafunzi anatakiwa kuja nayo wakati wa kuripoti shuleni ni kama ifuatavyo:-

1. Mwanafunzi anatakiwa aje na ufagio kwa ajili ya usafi wa mazingira.

CHAKULA CHA MCHANA

Mahitaji ya chakula cha mchana kinaratibiwa na Kamati ya chakula kilichochaguliwa na wazazi, hivyo; kwa muhula wa kwanza (1) Mwanafunzi anatakiwa aje na

(I) Mahindi **debe 2** kwa muhula anapo ripoti na **debe 3** $\frac{1}{2}$ kwa mwaka kuanzia **Julai 2021- June 2022.**

(II) Maharage **debe 1** kwa muhula anapo ripoti na **debe 1** $\frac{1}{2}$ kwa mwaka kuanzia **Mei 2021 - April 2022.**

FEDHA

Fedha kwa ajili ya kuni,mafuta ya kupikia, sukari, chumvi, vitunguu na kwa ajili ya kumlipia mpishi wa chakula cha wanafunzi ni kama ifuatavyo:-

KWA MUHULA	**KWA MWAKA**
Tsh.22,500/=	**45,000/=**

Fedha zote zinalipwa kwa kamati ya chakula na siyo kwa shule, na unatakiwa kuwasilisha stakabadhi ya benki kwa katibu wa kamati ya chakula siku unaporipoti na si fedha taslimu na fedha zote ziwekwe kwenye **Akaunti ya kamati ambayo ni GASECHA A/C. 41010006301**

Kila mwanafunzi aje na vyombo vya chakula, Sahani ya bati, Bakuli la bati na Kijiko na awe anavitunza vizuri na katika hali ya usafi wakati wote. Wanafunzi hawaruhusiwi kabisa kushirikiana vyombo wakati wa kula chakula.

N.B Nimarufuku mzazi kulipa fedha TASLIMU kwa Kamati kwani kufanya hivyo kunaweza kushawishi matumizi mabaya ya fedha, hivyo zilipwe BENKI

1. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na wizara ya elimu, mafunzo na sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais- Tamisemi yenye jukumu na usimamizi wa elimu, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi:-

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanya kazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kuandaa maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo kwa muda wote wa uanafunzi wako katika shule.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za shule.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUFUKUZISHA SHULE MOJA KWA MOJA

(a) Wizi

(b) Uasherati na ushoga

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine mirungi,kucheza kamali kama vile kubeti n.k.

(e) Kupigana na kupiga.

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

(g) Kudharau bendera ya Taifa.

(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba/kusababisha mimba.

(i) Kuoa au kuolewa.

(j) Kutoa mimba.

(k) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki vurugu na kuvunja amani na usalama wa shule au watu.

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi

(m) Kuwa na simu ya mkononi.

KARIBU SANA GABADAW SEKONDARI

…….

PONCIANI W. MAO

MKUU WA SHULE.

OFISI YA RAIS TAMISEMI

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

GABADAW SEKONDARI,

S.L.P 27,

KATESH- MANYARA.

TAREHE …….

FOMU NO.2

MKUU WA WILAYA,

S.L.P 10,

KATESH- HANANG.

YAH: UTHIBITISHO WA URAIA WA MWANAFUNZI

Ninaomba uthibitisho kwa mandishi kwamba mzazi/mlezi wa kijana mtajwa hapo juu ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba kijana wao ni mtanzania. (Kwa asiye na cheti cha kuzaliwa)

N.B: Ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa.

…….
MKUU WA SHULE

Ninathibitisha kwamba kuna ushahidi wa kutosha kuwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi.

……

(a) Raia wa kuzaliwa
(b) Si raia wa Tanzania

…….
MKUU WA WILAYA

MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

(FOMU YA MAPOKEZI SHULENI)

GABADAW
SEKONDARI
S.L.P 27
KATES- HANANG

SEHEMU A: IJAZWE NA MWANAFUNZI

Mimi…….. nakubali na kutii sheria zote za shule kama zilivyoanishwa hapo juu, sitashiriki katika migomo,fujo na makosa mengeine ya jinai.

Saini……..

Tarehe ……

SEHEMU B: IJAZWE NA MZAZI

1. Jina la mzazi……
2. Anwani ya Mzazi/mlezi……..
3. Mahali anapoishi(kijiji/kata)……
4. Kazi ya mzazi/mlezi…….
5. Mahali anapofanya kazi……
6. Ndugu wawili wa karibu(wanaoweza kufanya majukumu ya mzazi/mlezi kuhusu mwanafunzi).

NDUGU WA KWANZA.

1. Jina ……
2. Anwani……....
3. Uhusiano na mwanafunzi……...…….
4. Uhusiano wake na mzazi……..……....

NDUGU WA PILI

1. Jina ……
2. Anwani……
3. Uhusiano na mwanafunzi…….
4. Uhusiano wake na mzazi……..……..

SEHEMU C: IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

Mimi…….Mzazi/mlezi wa mwanafunzi……Ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatayotolewa na shule. **Na ahidi nitamsimamia mwanangu katika swala la mahudhurio kikamilifu na kuhakikisha mahitaji yake nayatimizi.**

Saini……

C. MEDICAL EXAMINATION FORM

PART I:

(To be completed by Medical Officer in Mission / Government Hospital)

Student's full name…… Age: ……. Date ……

I. a) Eye sight ……
b) Heart examination ……
c) Blood pressure: ……
d) Chest: ……
e) Hearing ……
f) Speech ……
g) Venereal diseases, Syphilis test ……
h) Leprosy ……
i) Sickle Cell test……
j) Asthma ……
k) HB ……
l) Epilepsy ……
m) Skin Diseases etc ……
n) T.B Test ……

II. Other serious diseases / Abnormalities ……
……

PART II:

I have examination the above named student and recommend that he/she is fit / unfit to join GABADAW Secondary School

Name and Signature of

Examiner ……

Designation ……

Station ……

Date ……

AGIZO: Mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu. Atakayegundulika shuleni kuwa hakuchukuliwa vipimo kihalali atarudishwa nyumbani kwa matatizo yatakayojitokeza kinyume na maoni ya daktari .